**HOTUBA YA KATIBU MKUU OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NDG. GEORGE D. YAMBESI KATIKA UFUNGUZI WA MKUTANO WA PILI WA BARAZA LA WAFANYAKAZI WA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI, ST. GASPAR DODOMA TAREHE 23-24 JANUARI, 2014.**

**Ndugu Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,**
**Ndugu Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma ,**
**Ndugu Mkurugenzi wa Manispaa ya Dodoma,**
**Ndugu Mwenyekiti wa TUGHE - Taifa,**
**Ndugu Mwenyekiti wa TUGHE - Mkoa wa Dodoma,**
**Ndugu Wajumbe wa Baraza,**
**Ndugu Wageni waalikwa,**
**Ndugu wanahabari,**
**Mabibi na Mabwana**

Habari za asubuhi, na Kheri ya Mwaka Mpya 2014.

**Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Baraza,**
Awali ya yote nachukua fursa hii kuwashukuru kwa kunialika kuwa mgeni Rasmi katika ufunguzi wa Mkutano huu wa pili wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, ambao kwangu umenipa fursa nyingine muhimu ya kukutana na Wawakilishi wa wafanyakazi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Naomba nichukue fursa hii kuwapa pole kwa safari kwani naelewa wengi wenu mmetoka katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, na

mmetumia muda mrefu njiani kuweza kufika kwenye mkutano huumuhimu na kushiriki,ili kufanikisha malengo ya Baraza. Tunamshukuru Mungu kwa kuwafikisha salama.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Naomba niwapongeze na kuwashukuru viongozi wa Mkoa wa Dodoma kwa kutukaribisha vema katika mji tulivu wa Dodoma. Nianze kwa kumshukuru Mkuu wa Mkoa, Katibu Tawala wa Mkoa, Meya wa Masipaa pamoja na Mkurugenzi wa Manispaa kwa ukarimu wao.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Mji wa Dodoma ni mji muhimu katika historia ya Nchi yetu. Rais wa awamu ya kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere aliwahi kuu-tamka Mji huu kuwa Makao Makuu ya Nchi yetu. Mji huu uko katikati ya Nchi yetu na tangu kuanzishwa kwake umekuwa ni mji umepangika vizuri . kimakazi na ki-Miundo Mbinu. Hivi sasa mji huu ni Makao Makuu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Mkoa wa Dodoma kwa ujumla wake unasifika sana kwa kilimo cha mizabibu na utengenezaji wa Mvinyo. Napenda kuupongeza uongozi wa Mkoa wa Dodoma na hasa Mamlaka na Ustawishaji Makao Makuu kwa jitihada kubwa za kuuboresha mji huu kiuchumi na maendeleo yanayoonekana siku hadi siku.

Pongezi zangu nyingine ni kwako wewe Mwenyekiti wa Baraza hili la Wafanyakazi la Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Ndugu Ludovick S.L. Utouh, kwa juhudi zako za kuijenga na kuiimalisha Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa kuzingatia ushirikishwaji wa wafanyakazi. Pia niwapongeze

wale wote waliohusika katika maandalizi ya Mkutano huu na shughuli nzima kwa ujumla.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ni kazi nyeti, si hapa Tanzania tu bali katika nchi zote zinazozingatia demokrasia,uwajibikaji na uwazi, katika mapato na matumizi ya rasilimali za umma ili kuleta maendeleo ya watu wake.

Jitihada na Mafanikio ya kazi za Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi yameijengea heshima nchi yetu na ulimwengu kwa ujumla. Hivi sasa Nchi yetu, ikiwakilishwa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, inakagua shughuli za Umoja wa Mataifa jambo ambalo ni la kujivunia sana. Niwapongeze watumishi wote wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa kazi nzuri mnayoifanya. Naomba kuwahakikishia kuwa Serikali inatambua juhudi mnazozifanya chini ya uongozi wako mahiri Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Kama unavyojua, ujenzi wa Taifa unahitaji ushirikishi wa wananchi katika kufanikisha malengo yaliyowekwa. Napenda kupongeza ofisi yenu kwani kwa kupitia ukaguzi shirikishi imewezesha kuboresha uandaaji na utoaji wa taarifa za mapato na matumizi ya Serikali kwa wakati, kwa ubora unaokubalika na kwa viwango vya kimataifa. Tumeshuhudia maboresho makubwa katika Taasisi za umma ambazo zimefuata ushauri wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ambapo tumeona kupungua kwa hati chafu au zenye mashaka katika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Matunda ya kazi

nzuri inayofanywa na ofisi hii yaonekana katika kupungua kwa kiwango kikubwa hoja za ukaguzi zinazoibuliwa katika kaguzi zenu. Hapa utaona uwiano mkubwa wa mafanikio ya kazi zenu unavyokwenda sambamba na Kauli Mbiu yenu yaani **“UKAGUZI SHIRIKISHI KWA MATOKEO MAKUBWA SASA”**.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Madhumuni ya Baraza la Wafanyakazi, kama wote tunavyoelewa, ni kutoa fursa kwa watumishi, kupitia wawakilishi wao, kujadiliana juu ya masuala mbalimbali ya msingi yanayohusu tija na ufanisi kwa upande mmoja na upande mwingine maslahi yao kama watumishi. Nimefurahi kusikia kuwa huu ni mkutano wa pili wa Baraza la Wafanyakazi katika Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2013/2014. Hii inaonyesha bayana namna ambavyo Menejimenti inatambua umuhimu wa watumishi kushirikishwa katika maamuzi yanayohusu taasisi yao kupitia Baraza la Wafanyakazi.Nawapongeza sana kwani uzoefu nilionao ni kuwa Mabaraza mengi hukutana mara moja kwa mwaka au hata kutokutana kabisa. Utaratibu wenu ni mzuri kwa sababu ni utaratibu unaoimarisha ushiriki wa kweli wa wafanyakazi katika uendeshaji wa shughuli za taasisi yao kama ilivyofafanuliwa katika sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma Sura 105. Napenda nichukue fursa hii nisisitize kuwa mikutano ya Baraza la Wafanyakazi itumike kujadili malengo na mipango ya taasisi ikiwa ni pamoja na Maslahi ya Watumishi. Mabaraza ya wafanyakazi yajadili utendaji wa kazi wa kila siku na jinsi ya kuboresha utendaji huo zaidi. Tija na maslahi lazima yawe na uwiano ili kuwa na matokeo ya utendaji kazi bora, unaolenga kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi tunaowatumikia. Tuelewe

kuwa, utendaji bora zaidi unaongeza tija, **tija** ikiongezeka ni rahisi kwa Serikali kuongeza maslahi ambayo hatimaye yanawawezesha watumishi kuishi maisha bora zaidi.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Baraza la Wafanyakazi mahali pa kazi lina wajibu mkubwa wa kuhakikisha kunakuwepo maelewano, ushirikiano na mshikamano kati ya wafanyakazi wa Uongozi wa Taasisi husika. Vile vile Baraza lihakikishe kuwepo kwa nidhamu ya kazi kwa madhumuni ya kuleta tija na ufanisi katika uendeshaji wa shughuli za taasisi.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi ambayo ina majukumu yaliyowekwa katika Katiba ya nchi na sheria nyingine zilizotungwa na Bunge. Ofisi imekuwa katika mstari wa mbele kutoa ushauri kwa Serikali ili kuongeza tija, hasa kupitia Kaguzi Yakinifu **- "Value for Money Audit**". Serikali imekuwa sikivu katika kutekeleza ushauri inayoupata kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,ili kusimamia vema rasilimali zinazohitajika kwa maendeleo ya Taifa letu. Kutokana na ushauri huo, mianya mingi ya upotevu wa mali na rasilimali za umma imezibwa na matokeo yake ni ongezeko la makusanyo ya mapato ya Serikali na kwa upande mwingine matumizi ya Serikali ambayo hayana tija kupungua. Nategemea kupitia Baraza hili na vikao vyenu vingine mtaendelea kuandaa mikakati ambayo itaboresha hayo mnayoyafanya.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Ili Taasisi yoyote iweze kutimiza majukumu yake kwa ufanisi ni muhimu kuwa na mazingira mazuri ya kazi yanayofaa. Wafanyakazi wanahitaji kupata ushirikiano toka kwenye uongozi, hali inayojenga uwezo wa wafanyakazi kupokea maelekezo, kuwa wabunifu na kuongeza ari na shauku ya kupata mafanikio makubwa zaidi. Kwa upande wa Serikali nikiwa Katibu Mkuu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ninaelewa liko suala la mishahara isiyokidhi uzito wa majukumu mliyonayo. Napenda kuwajulisha kuwa Serikali inatambua umuhimu wa kurekebisha mishahara yenu na ile ya watumishi wote na pindi hali ya uchumi itakapotengemaa marekebisho hayo yatapewa kipaumbele kinachostahili kama ambavyo Serikali imekua ikifanya mara kwa mara.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Katika Utumishi wa Umma hivi sasa liko changamoto kubwa la uzingatiaji wa Maadili ya Utumishi wa Umma. Naomba kupitia Baraza hili kusisitiza umuhimu wa Watumishi kufanya kazi kwa maadili na nidhamu ya hali ya juu. Kama wakaguzi wa utendaji wa Watumishi wengine wa Umma, watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni lazima waonyeshe mfano utakaoigwa na watumishi wengine wa Umma. Mkaguzi ni lazima uwe msafi zaidi kuliko unayemkagua. Nasisitiza hili kwa sababu ziko tetesi kuwa baadhi ya wakaguzi wa Mahesabu nao wanavunja maadili wakishirikiana na Wakaguliwa wenye utovu wa Maadili. Najua mna changamoto kubwa sana katika kazi zenu za Ukaguzi, nawaomba sana msikubali kuyumba daima muendelee kufuata misingi ya weledi na maadili katika utendaji kazi.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Kabla sijahitimisha hotuba yangu napenda nichukue fursa hii kuzungumzia suala zima kuhusu mapambano dhidi ya Rushwa. Sisi sote tunaelewa kuwa jitihada nyingi zimeendelea kufanywa na Serikali yetu,Taasisi na makundi mbalimbali katika jamii yetu ya Watanzania kuhusiana na mapambano dhidi ya rushwa. Kila mmoja wetu anajua fikakuwa **rushwa ni adui wa haki na maendeleo.**

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imebuni njia bora ya kuhakikisha inaziba mianya ya rushwa kwa kuwa na mfumo wa ukaguzi **shirikishi (Participatory audits).** Ukaguzi shirikishi ni dhana yenye kumshirikisha Mkaguzi na Mkaguliwa katika kuhakikisha wanafikia lengo moja la kuhakikisha matumizi sahihi ya fedha za Umma. Tunajua kuwa Taifa lenye maendeleo ni lile ambalo watu wake hufuata misingi ya Maadili na kutimiza wajibu wao. Hivyo basi nawaasa muendelee kushirikiana na Wakaguliwa katika kubuni mbinu bora zaidi za kutumia fedha za Umma kwa malengo ya maendeleo ya nchi yetu. Hatua hiyo itawasaidia pia Wakaguliwa kutoa ripoti zenye ubora na kupata hati safi.

**Ndugu Mwenyekiti,**

Matunda ya Mkutano huu, yanategemea sana mtakayoyajadili na kukubaliana kwa pamoja na kisha kuamua kuyatekeleza kwa ukamilifu. Mada mlizojipangia ni nzuri na za msingi kwa maendeleo ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Rai yangu kwenu ni kuwa Majadiliano yenu yatawaliwe na hekima, busara na uwazi, pia na pawepo maelewano. Nawaombeni nyinyi mliopata bahati ya kuwawakilisha

wenzenu muwe wawakilishi wazuri. Kuwepo kwenu hapa kumetokana na imani ambayo imejengeka kwa waliowachagua kuja kuwawakilisha. Mtakaporudi kwenye vituo vyenu vya kazi muitishe mikutano na kuwaelezea kwa kirefu mambo mtakayoafikiana katika mkutano huu kwa lengo la kujenga uelewa wa pamoja kwa taasisi nzima.

**Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Baraza,**

Baada ya kusema haya, naomba tena kuwashukuru kwa kunialika, na ni mategemeo yangu kuwa mtatumia vizuri nafasi yenu ya kuishauri Serikali kuhusu uboreshaji wa makusanyo ya mapato na matumizi ili Serikali iongeze uwezo wake wa kuwaletea wananchi maendeleo kwa haraka zaidi.

Baada ya kusema haya, sasa natamka kuwa Mkutano wa Pili wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, umefunguliwa rasmi.

**Ahsanteni kwa kunisikiliza**